# HAKI ZA MAZINGIRA, UHIFADHI NA UTUNZAJI MAZINGIRA TANZANIA

## UHALALI WA KUINGIZWA KWAKE KATIKA ITAKAYOKUWA KATIBA MPYA

# HAKI ZA MAZINGIRA, UHIFADHI NA UTUNZAJI MAZINGIRA TANZANIA

## UHALALI WA KUINGIZWA KWAKE KATIKA ITAKAYOKUWA KATIBA MPYA

**Oktoba, 2012**

## Wapitiaji wa Mada:

1. Dr. Tulia  Ackson
2. Bw. Hussein K. Mlinga
3. Dr. Deo Nangela
4. Bw. Elifuraha I. Laltaika
5. Bw. Ebenezar Mshana
6. Bi Asina A.Omari
7. Bw. Saudin J. Mwakaje

# Yaliyomo


1.0 Usuli ..... 1

2.0 Utangulizi ..... 2

3.0 Mantiki ya kuwa na Katiba inayozingatia Uhifadhi wa Mazingira..... 3

4.0 Haki za Mazingira, Uhifadhi na Utunzaji Mazingira Tanzania
Uhalali wa Kuingizwa Kwake Katika Itakayokuwa Katiba Mpya..... 5

5.0 Ufafanuzi wa Katiba yenye Kuzingatia Uhifadhi wa Mazingira..... 7

6.0 Haki za Mazingira, Misingi na Utaratibu wa Kisheria Tanzania..... 10

7.0 Tuliyojifunza Kutoka Katika Katiba za Nchi Zilizochaguliwa..... 13

8.0 Majumuisho na Mapendekezo ..... 16

a) Majumuisho ..... 16

b) Mapendekezo ..... 16

9.0 Bibliografia ..... 17

## Orodha ya Vifupisho

| | |
|---|---|
| ACTS | Kituo cha Kiafrika cha Mafunzo ya Teknolojia (African Centre for Technology Studies) |
| AIR | Taarifa Zote za India (All India Reports) |
| Cap | Sura (Chapter) |
| Eds | Wahariri (Editors) |
| EMA | Sheria ya Menejimenti ya Mazingira (Environment Management Act) |
| NEMC | Baraza la Taifa la Menejimenti ya Mazingira (National Environment Management Council) |
| SC | Mahakama ya Juu (Supreme Court) |
| UN | Umoja wa Mataifa (The United Nations) |
| UNCED | Mkutano wa Umoja wa Mataifa wa Mazingira na Maendeleo (United Nations Conference on Environment and Development) |
| USA | Shirikisho la Majimbo ya Amerika (United States of America) |

**Lawyers Environment Action Team(LEAT)**
P.O Box 12605
Dar es Salaam, Tanzania
Tel:+255 22 2781098
Mobile:0754 447323
Email: info@leattz.org
Website: www.leat.org.tz

**Policy Forum**
Plot 14, Sembeti Road
Off Old Bagamoyo Road.
Mikocheni B, P.O Box 38486
Tel: +255 22 2780200
Mobile: +255 782 317434
Email: info@policyforum.or.tz
Website: www.policyforum.or.tz

Mada hii imetayarishwa na Bw. E.S. Massawe wa "Lawyers Environmental Action Team".Shukrani za dhati zinatolewa kwa wafuatao walioshiriki katika kupitia hii mada: Dr. Tulia Ackson, Bw. Hussein K.Mlinga, Dr. Deo Nangela, Bw. Elifuraha I. Laltaika, Bw. Ebenezer Mshana, Bi Asina Omari na Bw. Saudin J.Mwakaje.

## Lawyers Association Action Team (LEAT)

Taasisi hii ya LEAT ni ya kwanza kuonyesha hadharani moyo wa kupenda kuingiza Sheria ya Mazingira Tanzania. Dhima yake ni kuhakikisha kuwa na mkakati imara wa menejimenti ya maliasili na uhifadhi wa mazingira nchini Tanzania. LEAT inajishughulisha na utafiti wa sera na utetezi kwenye baadhi ya maeneo ya maslahi ya umma yaliyochaguliwa. Washiriki wake kwa sehemu kubwa ni wanasheria wenye mwelekeo wa menejimenti ya mazingira na utawala wa kidemokrasia Tanzania.

## Policy Forum

Policy Forum ni mtandao wa Asasi zaidi ya 100 za kiraia za Tanzania zilizoungana pamoja kwa dhamira ya kushawishi michakato ya uundwaji sera ili kupunguza umaskini,kuleta usawa na demokrasia wakijikita zaidi katika uwajibikaji wa serikali kwa matumizi ya fedha za umma.

Tunapenda kutambua ufadhili wa kitaaluma na wa kifedha kutoka Shirika la "World Wildlife Fund – Coastal East Africa Network Initiative" Wakati wa kuelekea kuanza utafiti huu. Yaliyomo katika mada hii ni jukumu pekee la LEAT na Policy Forum na kwa hali yoyote ile hayawezi kuhusishwa na nafasi za wale waliofadhili kazi hii.

*Katiba iko juu ya yote, ni sheria mama inayohakikisha haki msingi ya mtu binafsi na haki za pamoja na uhuru, inayolinda msingi wa uhuru wa watu kuchagua na inayotoa uhalali wa matumizi ya madaraka. Inasaidia kuhakikisha ulinzi wa kisheria na udhibiti wa mamlaka ya umma katika jamii ambapo sheria inazingatiwa na maendeleo ya binadamu yanapewa kipaumbele katika nyanja zote.*

*- Utangulizi, Katiba ya Algeria[1](1996)*

## 1. Usuli

Mada hii inalenga katika kuchochea mjadala na kutoa taarifa zaidi katika mchakato unaoendelea wa kupata katiba mpya ya Jamhuri wa Muungano wa Tanzania. Inatoa majumuisho (usanisi) ya mapitio ya katiba ya sasa ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Katiba za baadhi ya nchi zilizochaguliwa ambazo zimezingatia haki za mazingira, uhifadhi na menejimenti yake. Mapitio hayo yanadokeza uingizaji wa vipengele vya haki za mazingira, uhifadhi na manejimenti yake katika itakayokuwa - katiba mpya. Mada hii inatoa mapitio na mapendekezo juu ya nini kifanyike ili kuhakikisha kuwa mambo ya msingi yameingizwa katika itakayokuwa katiba mpya.

Malengo mahususi ya mada hii yako katika sehemu mbili: Kwanza ni kuwaarifu wadau na kuinua ufahamu wao juu ya maudhui ya mada hii ili waweze kutoa mchango wao ipasavyo katika mchakato wa uandaaji wa katiba na mijadala husika. Pili, mada hii inatafuta kujenga msingi wa kisheria wa kuingiza vipengele vitakavyoweza kushughulikia ipasavyo masuala yote yenye uhusiano na haki za mazingira, uhifadhi na menejimenti yake katika itakayokuwa Katiba Mpya ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Sambamba na maelezo yaliyotangulia, inatarajiwa kuwa harakati za wadau kitaifa zitatoa jukwaa pana kwa ushiriki mkubwa zaidi katika mijadala kuhusu uingizaji wa haki za mazingira, uhifadhi na menejimenti ya mazingira katika itakayokuwa katiba mpya. Pitio hili linategemewa kuwafahamisha wananchi masuala muhimu kuhusu haki za mazingira, uhifadhi na menejimenti yake, hivyo kuwawezesha kutoa maoni bora na mchango wao katika mchakato wa uandaaji wa Katiba.

1 *Katiba ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Algeria, 1989 (iliyorekebishwa kwa mapitio ya katiba ya mwaka 1996)*

## 2.0 Utangulizi

Tanzania ni nchi ambayo kwa sehemu kubwa ni yenye mazingira ya asili yenye kuvutia na mandhari yenye ujazo upatao kilomita za mraba 945,000[2] Mandhari hii imegawanyika katika maeneo ya bahari, maziwa, ardhi inayolimika na isiyolimika, vilima na milima. Katika mada hii neno mazingira linamaanisha vinavyotuzunguka ambavyo vinajumuisha: ardhi, hewa, anga, maji, bio-anwai, wanyama pori misitu, rasilimali madini, wanadamu, na mfumo-ekolojia katika ujumla wake. Mahusiano kati ya yote yaliyotajwa ndiyo yanatengeneza mazingira.

Menejimenti ya mazingira inaweza kufuatiliwa kurudi nyuma mpaka pale uhai wa binadamu ulipoanza. Mifumo, matumizi bora na taasisi ziliwekwa kusimamia na kuiangalia menejimenti ya mazingira katika sehemu mbalimbali za dunia, ikiwa ni pamoja na Tanzania. Hata hivyo, kabla ya Mkutano wa Umoja wa Mataifa wa Mazingira ya Mwanadamu wa mwaka 1972, menejimenti ya mazingira ilikuwa haijaliwi sana, na ilikuwa ni suala lililowekwa pembezoni tu[3]. Mkutano huo ulikuwa wa kwanza kimataifa kuandaliwa ili kuzungumzia matatizo ya mazingira kiulimwengu. Kuanzia hapo menejimenti ya mazingira imekuwa ni ajenda ya kiulimwengu sambamba na maendeleo. Mkutano huu wa kimataifa uliweka misingi ya menejimenti ya mazingira na msingi wa maendeleo endelevu.

Baada ya miaka ishirini (1992), Mkutano wa Umoja wa Mataifa kuhusu mazingira na Maendeleo (UNCED) ulifanyika katika Jiji la Rio de Janeiro, nchini Brazil. Wakati wa Mkutano huo (UNCED) Umoja wa Mataifa ulitafuta namna ya kusaidia Serikali za nchi kufikiria kwa upya maendeleo yao ya kiuchumi, na kutafuta mbinu za kuzuia uharibifu wa rasilimali asili isiyoweza kurejeshwa, mazingira na uchafuzi wa sayari yetu[4]. Mikutano hii ya kimataifa juu ya Mazingira imekuwa majukwaa ya kufanyia maamuzi ya kimataifa kuhusu menejimenti ya mazingira ulimwenguni. Maamuzi ya kimataifa yaliyofikiwa wakati wa mikutano mikuu ya kiulimwengu yameleta mabadiliko makubwa katika menejimenti ya mazingira katika nchi wanachama wa Umoja wa Mataifa. Katika muongo uliopita, tumeshuhudia mabadiliko mengi kiulimwengu na kitaifa, yakishinikiza serikali ziweke mkazo zaidi katika menejimenti ya mazingira na kuweka juhudi za makusudi katika kushughulikia matatizo ya

2 *TAZAMA, http://www.state.gov/r/pa/ei/bgn/2843.htm, ya tarehe 22/12/2011*
3 *http://www/.worldsummit2002.org/index.htm?http://www.worlsummit2002.org/guide/stockholm.htm, ya tarehe 26/12/2011*
4 TAZAMA, Mkutano wa Umoja wa Mataifa kuhusu Mazingira na Maendeleo, katika :http://www.un.org/geninfo/bp/enviro.html, ya tarehe 26/11/2011

kimazingira. Juhudi hizi za kiulimwengu na za kitaifa ni za kupongezwa sana kwa kuwa hatimaye zimeleta mabadiliko makubwa kisheria na kitaasisi ambayo matokeo yake yanaonekana wazi. Sambamba na hili na kwa kutumia fursa ya mapitio yanayoendelea ya katiba na michakato yake iliyoanzishwa Tanzania, wahifadhi na wana mazingira wanajenga ushirika, wakishirikiana kirasilimali na kitaalamu katika kampeni ya utetezi wa uingizwaji wa masuala yanayohusu haki za mazingira, uhifadhi na menejimenti yake katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Ni kwa kuzingatia haya yaliyoelezwa katika usuli na utangulizi huu, kwamba watu, taasisi, na mashirika yanayoshughulika na mazingira yanachukua hatua chanya kujadili kwa kina, kuinua ufahamu wa watu na kuendesha kampeni ili kujenga umma makini na hivyo kuwezesha raia kumiliki mchakato na kushiriki kikamilifu katika mchakato wa mapitio ya Katiba unaoendelea na katika utayarishaji wake.

## 3.0 Mantiki ya Kuwa na Katiba Inayozingatia Uhifadhi wa Mazingira

Kwa kuzingatia sheria nyingi za mazingira, kanuni na viwango vilivyopo na vinavyoandaliwa katika nchi nyingi za kiafrika, ni busara kufikiria kuingiza vifungu hivi ndani ya katiba ili kuhifadhi na kusimamia mazingira. Kwa kuzingatia mwamko wa ufahamu wa mazingira katika miongo ya hivi karibuni, mazingira yamekuwa ni suala la kipaumbele katika siasa na katiba nyingi sasa zinatoa hakikisho la "haki ya mazingira bora" pamoja na haki za taratibu zinazohitajika katika utekelezaji na uhimizaji wa haki muhimu zilizotolewa[5]. Vifungu vya Katiba vinavyoainisha haki za msingi za raia, siyo mara zote vimekuwa moja kwa moja chini ya uwezo wa raia kuhakiki utekelezaji wake na siyo mara zote vimejenga thibitisho la haki. Hata hivyo mwelekeo wa kimataifa ni katika kuimarisha upatikanaji wa haki zilizoainishwa katika vifungu hivi[6].

[5] Bruch, C. et al, (2001), "Breathing Life into Fundamental Principles: Implementing Constitutional Environmental Protections in Africa", in Ribot, J. C. and Veit, P. G., Environmental Governance in Africa, Working Paper Series, World Resources Institute, Washington D.C., USA, p.5, accessed at http://pdf.wri.org/eaa_bruch.pdf. Also in "Call to include Environmental Rights in the Constitution", The Citizen Newspaper, 22 June 2011, at p. 22.,
[6] Ibid,

Uingizwaji wa vifungu hivi katika katiba kunaweza kuimarisha kwa kiwango kikubwa uwezo wa mawakili kutumia sheria kulinda haki za mazingira kwa njia mbalimbali. Kwanza wanaweza kupanua upeo wa sheria ya mazingira na kanuni na taratibu zake ambazo mara nyingi ufafanuzi wake hautoshelezi kuleta uhifadhi unaotosheleza. Hata nchi zenye mifumo iliyoendelea hukuta kuwa sheria zao hazijajielekeza katika kufanyia kazi masuala yote yahusuyo mazingira. Uwepo wa vifungu hivi katika katiba unaweza kutoa fursa salama ya kutatua matatizo ya kimazingira ambayo mifumo ya sheria na kanuni zilizopo haziwezi kutatua[7].

Pili katiba yenye vifungu vinavyozingatia suala la mazingira, inaweza kuinua ulinganifu wa hadhi ya haki za mazingira, ambayo mara nyingi inawekwa nafasi ya nyuma inapolinganishwa na vipaumbele vingine kama vile maendeleo ya uchumi. Kwa kurejea uhifadhi wa kimazingira ulioainishwa katika katiba, mawakili wanaweza kuzipandisha daraja mashauri (kesi) ya kimazingira yakawa mashauri ya kikatiba yenye kuzingatia haki msingi za binadamu[8]. Zaidi ya hayo uingizwaji wa haki za kimazingira, uhifadhi na menejimenti yake katika katiba hutoa uwanja madhubuti kwa uhifadhi wa mazingira ambao si rahisi kuingiliwa kisiasa. Matokeo yake ni kwamba hali ya watu kuthamini mazingira itakuwa endelevu zaidi kwani mabadiliko ya katiba yanahitaji kazi kubwa, ni vigumu na huhitaji ukubali wa wengi ili kupata idhini[9].

Mwishoni, Katiba mara nyingi ni chanzo cha taratibu za haki zinazohitajika kwa asasi za kimazingira na asasi nyingine za kiraia kuendesha shughuli zao za utetezi. Uimarishaji wa vifungu vya katiba vinavyohakikisha upatikanaji wa taarifa, ushiriki wa umma, na msimamo wa kimahakama katika masuala ya kimazingira, ni muhimu katika kuhakikisha kuwa haki stahiki za watu kuhusu maisha na mazingira bora zinalindwa[10].

---

[7] Ibid.,

[8] Tumushabe, G.W., (1999), "Environmental Governance, Political Change and Constitutional Development" in Uganda in Okoth-Ogendo, H. W. O. and Tumushabe, G.W., (Eds), Governing the Environment: Political Change and Natural Resources Management in Eastern and Southern Africa, African Centre for Technology Studies (ACTS), Nairobi, Kenya, pp. 63-88, at p. 78. Also in, Bruch, C., et al, (2001), "Breathing Life into Fundamental Principles: Implementing Constitutional Environmental Protections in Africa", in Ribot, J. C. and Veit, P. G., (Eds) Environmental Governance in Africa, Working Paper Series, World Resources Institute, Washington D.C., USA, p.5.

[9] Bruch, C., et al, (2001), Op. Cit., p.6.

[10] Ibid.,

## 4.0 Haki za Mazingira, Uhifadhi na Utunzaji Mazingira Tanzania Uhalali wa Kuingizwa Kwake Katika Itakayokuwa Katiba Mpya

Kabla ya kupitishwa kwa sheria ya Menejimenti ya Mazingira ya mwaka 2004, jumla ya sheria za Tanzania, zile zinazotoa haki kwa mazingira safi na yenye afya zilikuwa hazina msingi imara. Mara kadhaa, mahakama nchini Tanzania zililazimika kutafuta miongozo kutoka nchi nyingine ambazo ni wanachama wa Jumuiya ya Madola, katika kutafuta uhalali wa kuwapa walioleta shauri la pingamizi ahueni katika mchakato wa ubishani wa shauri la kimazingira mahakamani[11]. Kwa hali hii, ilibidi mahakama zikimbilie kwenye katiba yenye vifungu vilivyo wazi vinavyohakikishia wananchi haki ya mazingira masafi na yenye afya bora.

Katika baadhi ya kesi majaji walipata ugumu wa kutumia vifungu vya katiba ya nchi nyingine na walijaribu kutafsiri vifungu vya katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 ili kuhalalisha maamuzi yao dhidi ya walioleta shauri la pingamizi ambao haki zao za kimazingira zimekiukwa[12]. Hii ilikuwa kazi ngumu na ilifanywa ngumu zaidi kwa kuwa mshauri alitoa msaada kidogo sana katika kuandaa kwa maarifa ya kisheria ubishani wa shauri la kimazingira mahakamani kwa kuzingatia mfumo wa sheria ya Tanzania. Kutokana na kutokuwepo kifungu mahususi kinachohakikisha haki ya mazingira masafi na yenye afya, kifungu cha katiba kilichotegemewa sana na mahakama kilikuwa ni kile kilichotoa haki ya kuishi. Mahakama zilijitahidi kutafsiri kifungu hiki kadiri walivyoweza ili kuhalalisha maamuzi yao.

Mfano halisi ni ubishani na uamuzi uliotolewa katika shauri la Festo Balegele na wengineo 794 dhidi ya Halmashauri a Jiji la Dar es Salaam [13]. Kwa kadiri ya shauri hili mtu binafsi hakuwa na mamlaka ya kisheria kufungua shauri mbele ya mahakama kama siyo waathirika wa moja kwa moja au wadhurika wa jambo husika. Mahakama kuu katika shauri hili ilitoa hukumu inayokubaliana na Wadai (Festo Balegele na wengine) kwa kuonesha kuwa wadai ni wadhurika wa moja kwa moja na utupaji wa taka kule Kunduchi Mtongani. Hii iliwapa Wadai mamlaka ya kisheria kwa mahakama kuendelea na shauri la pingamizi kwa stahili. Wakati pingamizi kuhusu shauri hili lilipoletwa, watu hawakuwa na haki ya kuleta shauri kuhusu mazingira nchini

[11] Festo Balegele and 794 Others v. Dar es Salaam City Council, High Court of Tanzania at Dar es Salaam, Miscellaneous Civil Cause, No. 90 of 1991

[12] Ibid.,

[13] Mahakama Kuu ya Tanzania, Dar es Salaam, Miscellaneous Civil Case No. 90 of 1991

Tanzania na hapakuwa na kifungu chochote kinachohusu " Haki ya kuishi katika mazingira masafi na yenye afya" iliyowekwa katika sehemu yoyote ya sheria.

Ni muhimu kutambua kuwa, siyo majaji wote walikuwa wabunifu wa kutumia mbinu hii, hivyo kuacha haki za wanaoleta pingamizi la shauri katika hali ya mashaka. Kwa ulinganisho katika maeneo ambapo haki ya kuishi katika mazingira masafi na yenye afya imeingizwa katika katiba, mahakama zilikuwa na kazi rahisi na mashauri ambapo haki za wananchi za mazingira zilikiukwa yaliweza kushughulikiwa kwa wepesi.

Ingawa hukumu katika shauri la Festo Balegele imeweka msingi wa pingamizi la shauri kwa mashauri ya kimazingira kwa kutoa mamlaka ya kisheria na kutambulisha haki ya kuishi katika mazingira masafi na yenye afya hapa Tanzania, inazibana tu mahakama zilizo chini ya mahakama kuu. Katika hali ambapo shauri linalofanana na hili litakapofunguliwa mbele ya Mahakama kuu, Jaji atakayesimamia shauri hilo atakuwa na uhuru wa kuifuata au la. Hii ni kwa sababu kwa kuzingatia msingi wa "ngazi za maamuzi" mara tu mahakama iliyo katika ngazi ya juu ikipitisha maamuzi, mahakama zote zilizo chini yake zinalazimika kufuata maamuzi kutoka juu.

Kifungu chenye uhusiano wa namna fulani na menejimenti ya mazingira kiliingizwa kupitia kifungu cha Muswada wa Sheria wa Haki za Binadamu wakati wa marekebisho ya katiba yaliyopitishwa mwaka 1984. Hii imeainishwa kwenye ibara ya 14, inayosema kwamba kila mtu ana haki ya kuishi na ya kupata ulinzi wa maisha yake kutoka kwa jamii. Hiki ni kifungu ambacho Mahakama Kuu ya Tanzania ilikazana kutafsiri katika kutoa hukumu ya haki za kimazingira.

Katika jitihada ya kujaza pengo hili la kikatiba waandishi wa rasimu ya Sheria ya Mazingira[14] (Environmental Management Act – EMA) ya mwaka 2004, waliingiza kifungu kwenye sheria hiyo kinachoainisha "Haki ya Mazingira masafi na yenye afya". Ingawa huu ni ubunifu mzuri, hauna mizizi katika katiba, hivyo kuiacha idara ya mahakama katika hali tatanishi kuhusu misingi ya kisheria ya kifungu hiki ndani ya sheria mama ya nchi (katiba), jambo ambalo wakati mwingine haliwezi kuhakikisha matokeo ya jinsi hakimu binafsi atakavyotafsiri shauri lililoletwa mbele yake. Hii ni kwa sababu mahakama za sheria zinaweza kutoa tafsiri tofauti tofauti kwenye kifungu hiki.

[14] Sheria, Na. 20 ya 2004

Katika hali ambapo kifungu hicho kimeainishwa kwa umakini katika Katiba, hali isingekuwa hivyo. Pia, ni rahisi zaidi kubadilisha kifungu maalum cha sekta ya sheria ambayo inaweza kuathiri haki ya watu kufikia, kuhifadhi na kutunza mazingira. Kwa upande mwingine, siyo rahisi kubadilisha vifungu vya Katiba kuathiri haki ya watu kufikia, kuhifadhi na kutunza mazingira iliyotolewa kwa raia. Hii ni kwa sababu tukio la marudio ya urekebishaji wa katiba mara nyingi huamuliwa na hali ya uhitaji wa haraka kulikoni utaratibu wa kawaida.

Kuna hitaji la muhimu kuingiza vifungu maalum vinavyohusu haki za mazingira, uhifadhi na menejimenti ya mazingira katika itakayokuwa katiba mpya**.** Hii italinda dhidi ya uwezekano wa kupitisha sheria za kisekta au urekebishaji wa sheria zilizopo kwa namna ambayo inadhoofisha haki ya kufikia, kuhifadhi, na kutunza mazingira iliyotolewa kwa wananchi.
Hii inaendana na kanuni ya kuwa Katiba ni sheria kuu ambayo sheria nyingine zote sharti zikubaliane nayo.

Kwa hali inayojitokeza ya msukumo kuelekea kwenye muungano wa nchi za Afrika ya Mashariki, masuala ya ufikiaji, uhifadhi, na utunzaji wa mazingira katika baadhi ya nchi[15] yametawala majadiliano. Kwa matokeo, hii imefanya baadhi ya nchi katika ukanda huu kuingiza vifungu maalum katika katiba zao kuhusu haki za watu kuhifadhi na kutunza mazingira[16].

## 5.0 Tafsiri ya Vifungu vya Katiba ili Kuhifadhi Mazingira.

Kama ilivyojadiliwa katika sehemu ya tatu hapo juu, Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 (kama ilivyorekebishwa kwa nyakati mbalimbali) inayo vifungu ambavyo ingawa havionyeshi waziwazi uhifadhi na menejimenti ya mazingira, vina uhusiano nayo. Kutokana na ukosefu wa vifungu vinavyoainisha waziwazi haki ya ufikiaji, uhifadhi na menejimenti ya mazingira katika katiba, mahakama zimekuwa na wakati mgumu katika utoaji wa tafsiri toshelevu wa haki hizo ikiwa ni pamoja na haki ya kuishi katika mazingira masafi na yenye afya[17].

15 Hali hii ilijitokeza wakati wa utayarishaji wa Katiba ya Kenya na imeanzishwa nchini Tanzania
16 TAZAMA, sura ya tano ya Katiba ya Jamhuri ya Kenya ya mwaka 2010
17 Ikumbukwe kwamba hii inazungumzia kipindi cha kabla ya 2004 wakati Tanzania haikuwa na mfumo wa kisheria kuhusu uhifadhi na menejimenti ya mazingira

Kwa ujumla sheria zilizotumika kudhibiti masuala ya kimazingira zilikuwa sheria za kisekta zilizotumika kwa pamoja na Sheria ya Kitaifa ya Baraza la Utunzaji wa Mazingira ya mwaka 1983 iliyoanzisha Baraza la Taifa la Utunzaji wa Mazingira (NEMC)

Wakati jambo linalohusiana na tafsiri ya sheria kuhusu uhifadhi na menejimenti ya mazingira na haki ya kuishi katika mazingira masafi na yenye afya lilipoletwa mahakamani, majaji waliegemea kwenye yaliyomo katika ibara ya 14 ya katiba. Ibara ya 14 ya katiba inatoa haki ya kuishi. Hii ilitafsiriwa kutoa uamuzi kuhusu haki ya kuishi katika mazingira safi na yenye afya. Tafsiri isiyofupishwa ya ibara ya 14 ya katiba katika Kiswahili inatamka kwamba:

> "*Kila mtu anayo haki ya kuishi na kupata kutoka kwa jamii hifadhi ya maisha yake, kwa mujibu wa sheria.*"

Tafsiri ya vifungu vya katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania vyenye uhusiano na uhifadhi na menejimenti ya mazingira kusingeleta utata kwa majaji kama kungekuwa na vifungu vinavyoainisha kwa umakini kuhusu masuala haya**.** Ni bora kutambua kuwa kwenye mashauri ambapo hakuna kifungu cho chote katika sheria za kitaifa na katika katiba kinachodhamini uhifadhi na utunzaji wa mazingira, hakuna shaka kuwa uharibifu wa mazingira unaweza kuachwa uendelee bila kukoma na hatimaye kuhatarisha maisha ya vizazi vya sasa na vijavyo.

Katika mamlaka nyingine za kisheria hali haikuwa tofauti sana na ya Tanzania, ambapo hapakuwa na kifungu katika katiba chenye kueleza kwa uwazi uhifadhi wa mazingira. Nchini India kwa mfano, haki ya kuishi imetumika katika namna tofauti tofauti. Inajumuisha pamoja na mambo mengine, haki ya kuishi kama viumbe hai, thamani ya maisha, haki ya kuishi kwa heshima na haki ya kupata riziki. Lakini, aina na upeo wa haki hii siyo sawasawa na haki ambayo inaweza kutekelezwa kibinafsi na yenye kuelekeza kwenye ekolojia nzuri na yenye afya kama ilivyoainishwa katika Katiba ya Ufilipino (Philippines)[18].

[18] TAZAMA, Human Rights and the Environment:the national experiencein South Asia and Africa at: http://www2.ohchr.org/english/issues/environment/environ/bp4.htm, accessed on 10/01/2012.

[19] Maneka Gandhi v. Union of India, AIR 1978 SC 597, 623-624.

Ibara ya 21 ya Katiba ya India inatamka kuwa, "Hakuna mtu atakayenyimwa maisha yake au uhuru binafsi isipokuwa kwa taratibu na kanuni zilizowekwa kisheria". Mahakama Kuu ya India ilipanua hii haki hasi kwa njia mbili. Kwanza, sheria yo yote inayugusia uhuru binafsi lazima iwe yenye mantiki, isiyobagua na ya haki[19]. Pili, Mahakama ilitambua uhuru/haki nyinginezo ambazo hazikuwekwa katika maandishi zilizomaanishwa na ibara ya 21. Ni kwa njia hii ya pili kwamba Mahakama kuu ilitafsiri haki ya maisha na uhuru binafsi kujumuisha haki ya mazingira masafi[20].

Nchini India uhusiano kati ya ubora wa kimazingira na haki ya kuishi ilizungumziwa kwa mara ya kwanza kikatiba katika Baraza la Mahakama ya Juu Katika shauri la Charan Lal Sahu dhidi ya Umoja wa India[21]. Mwaka 1991, Mahakama ya Juu Ilitafsiri haki ya maisha inayohakikishwa na ibara ya 21 ya Katiba ya India kujumuisha haki ya kuwa na mazingira bora.

Katika shauri la Subash Kumar[22], mahakama ilizingatia kwamba haki ya kuishi inayodhaminiwa na ibara ya 21 inajumuisha haki ya kufurahia maji na hewa yaliyo huru na uchafuzi ili kufurahia maisha[23]. Bila shaka, katika hali ya kutokuwepo msingi imara katika katiba unaotoa haki za mazingira, uhifadhi na menejimenti ya mazingira, kuna uwezekano mkubwa sana kwamba hizi haki zitatafsiriwa kitofauti na mahakama mbalimbali pale shauri litakapofunguliwa katika mahakama mbalimbali za sheria. Uingizaji katika katiba wa vifungu maalum vilivyoainishwa kwa umakini na kwa uwazi kuhusu haki za mazingira, uhifadhi, utunzaji na usimamizi wa mazingira kutasaidia kulinda haki za watu na kuzuia uharibifu wa mazingira.

[19] *http://www2.ohchr.org/english/issues/environment/environ/bp4.htm,* accessed on 10/01/2012.

[20] AIR 1990 SC 1480.

[21] Subhash kumar v. State of Bihar, AIR 1991 (1) SCC 598.

[23] http://www2.ohchr.org/english/issues/environment/environ/bp4.htm, accessed on 10/01/2012

## 6.0 Haki za Mazingira, Misingi na Utaratibu wa Sheria Tanzania

Ili kujaza pengo la kisheria, mwaka 2004 Tanzania ilipitisha mfumo wa kisheria iliyoitwa Sheria ya Menejimenti ya Mazingira (Environment Management Act – EMA) ili kuratibu uhifadhi na menejimenti ya mazingira. Mbali na kuwa na vifungu makini na vinavyoeleweka kuhusu uhifadhi na menejimenti ya mazingira, hii sheria inatoa haki na jukumu kwa raia binafsi kuhifadhi, kusimamia na kutunza mazingira. EMA imeweka msingi wa kuwa na sheria mahali pake ikiwa na vifungu wazi na makini kuhusu uhifadhi na menejimenti ya mazingira.

EMA inawezesha mfumo wa kisheria na wa kitaasisi unaotoa mwongozo kuhusu menejimenti endelevu ya mazingira, kanuni ya usimamizi na utunzaji wa mazingira, misingi ya utekelezaji wa hati rasmi za kimataifa kuhusu mazingira na wa sera ya Taifa ya mazingira. Zaidi ya yote EMA inatoa haki za mazingira kwa watu binafsi wenye kuathiriwa au wenye maslahi yoyote kuhusu suala lolote la kimazingira na mamlaka ya kisheria kwa watu binafsi[24] na asasi za kiraia kufungua shauri la kimazingira kwa niaba ya wengine kwa kuwasaidia wao kudai haki zao za kimazingira pale zinapokandamizwa.

Kabla ya EMA kuundwa, haki za mazingira, uhifadhi na menejimenti ya mazingira zilikuwa hazijainishwa vizuri katika vifungu vya sheria za kisekta. Masuala ya menejimenti ya mazingira yalikuwa yameainishwa kupitia mtazamo wa kisekta tu na vipengele mbalimbali vya kisheria vilitayarishwa kurekebisha menejimenti ya misitu[25], wanyama pori[26], raslimali maji[27], madini[28], na ardhi[29]. Ingawa vyote hivi ni sehemu na kifungu cha mazingira, Tanzania ilikuwa haina vifungu vilivyoainishwa kwa uwazi na kwa umakini kuhusu haki za mazingira na misingi ya menejimenti ya mazingira endelevu. Kwa hali hii, kwa hiyo kulikuwa na uhitaji muhimu wa kutunga sheria itakayosimamia haya.

[24] TAZAMA, sehemu ya tano ya Sheria ya Menejimenti ya Mazingira (EMA), Na 20 ya 2004
[25] Sheria ya Misitu ya 2002
[26] Sheria ya Uhifadhi wa Wanyama Pori, Sura. 283
[27] Sheria ya Matumizi ya Maji (Udhibiti na Utaratibu), Sura 331, Waterworks Sura. 272
[28] Sheria ya Madini, Sura. 123
[29] Sheria ya Ardhi, Sura. 113 na Sheria ya Ardhi ya Kijiji Sura. 114

Utungaji wa sheria iliyounda EMA ulichukua mawazo kutoka hati rasmi za kimataifa na maamuzi yaliyofanywa na jumuiya za kimataifa. Pia ulichukua vifungu vilivyoko katika hati za Kikanda zinazohusu mazingira. Kwa kuwa EMA ni sheria mfumo, na kwa kuzingatia kwamba utungaji wa sheria nyingine za kisekta zinazoratibu sekta zenye uhusiano na mazingira ulishafanyika, waandaaji wa rasimu ya sheria hiyo, waliweka kifungu katika sheria inayoifanya EMA kuwa sheria kuu katika masuala ya mazingira, ikiwa kuna mikanganyo au utata na vifungu vya sehemu nyingine za sheria[30].

Licha ya utoaji wa vifungu wazi na makini kuhusu haki ya kiutendaji[31] katika suala la mazingira na wajibu wa kuhifadhi mazingira[32], EMA inatoa kanuni za msingi[33] za menejimenti ya mazingira. Kanuni hizi ni:-

(a) Kanuni ya tahadhari, inayotaka kwamba pale ambapo kuna hatari kubwa ya uharibifu ambao hauwezi kurekebishwa kutokea, ukosefu wa uthibitisho wa kisayansi usizuie au kudhoofisha uchukuaji wa hatua za tahadhari ili kuhifadhi mazingira

(b) Madhara makubwa yazuiliwe au kupunguzwa kupitia mipango ya pamoja na uratibishaji, mfungamano/ushirikiano na juhudi za pamoja zinazochukulia mazingira yote katika ujumla wake.

(c) Kanuni ya mchafuzi kulipa gharama, ambayo inataka mtu yeyote anayesababisha madhara makubwa kwenye mazingira kulipa kikamilifu gharama za kijamii na za kimazingira za kuepusha, kupunguza na / au kurekebisha athari hizo.

(d) Kanuni ya ushiriki wa umma, inayotaka uhusishaji wa watu katika uandaaji wa sera, mipango na michakato ya menejimenti ya mazingira.

(e) Ufikiaji wa taarifa za kimazingira, zinazowezesha raia kufanya uchaguzi binafsi ulio makini na unaoboresha utendaji katika viwanda na serikali

30 Sehemu ya 232:" Pale ambapo kifungu chochote katika hii sheria (EMA) kina utata (EMA) kwa namna fulani hakiendani na kifungu au sheria nyingine yoyote iliyoandikwa inayohusu menejimenti ya mazingira, kifungu cha sheria hii (EMA) kitatumika kwa kadiri ya huko kutoendana

31 Sehemu ya 5 ya Sheria ya Menejimenti ya Mazingira (EMA), Na 20 ya 2004

32 Sehemu 6, ibid.,

33 Sehemu 7, ibid.,

(f) Ufikiaji wa haki, ambao unawapa watu binafsi, umma na vikundi kereketwa fursa ya kulinda haki zao za ushiriki na kupinga maamuzi yasiyozingatia maslahi yao.

(g) Uzalishaji wa taka upunguzwe, pale inapowezekana taka lazima, kwa kuzingatia kipaumbele, zitumike tena, zizungushwe, zipatikane tena na ziondolewe kwa usalama kwa namna ambayo haitaleta athari kubwa au kama hii haiwezekani kuepukwa, kwa hali ambayo ina uwezekano mdogo wa kuleta athari kubwa.

(h) Kanuni ya usawa katika mwingiliano wa vizazi, ambayo inataka matumizi ya maliasili isiyorudishika yafanyike kwa uangalifu mkubwa, kwa kuzingatia matokeo yake kwa kizazi cha sasa na vizazi vijavyo.

(i) Kanuni ya matumizi endelevu, ambayo inataka maliasili inayorudishika na mfumo ekolojia vitumike tu kwa namna ambayo ni endelevu na isiyoathiri uwezo wao wa kuendelea kuishi au kumea kwa ukamilifu.

Kanuni zote za menejimenti ya mazingira zilizotajwa hapo juu ni za manufaa sana kwa ulinzi, uhifadhi, utunzaji na usimamizi wa mazingira. Kwa hali hii, inashauriwa kuwa hazina budi ziingizwe katika itakayokuwa Katiba mpya ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ili kuwe na mamlaka yenye nguvu katika kuhakikisha utekelezaji wake.

Zaidi ya hayo, ni vizuri kutambua kuwa utungaji wa sheria iliyounda EMA na upinzani wa kisheria wa mashauri (kesi) ya kimazingira kabla ya mwaka 2004, umechangia kwa kiwango kikubwa katika ukuzaji wa falsafa ya sheria ya mazingira nchini Tanzania. Tanzania ilikuwa na idadi ndogo ya wataalam wa sheria ya mazingira kwa muda mrefu. Hii ni kwa sababu sheria ya mazingira haikufundishwa katika chuo kikuu kama somo la lazima au la hiari. Wataalamu wachache wa sheria ya mazingira waliopo Tanzania kabla ya mwaka 2000 walisomea nje ya nchi.

Ni katika miaka ya mwanzo ya 2000, ndipo sheria ya mazingira ilipoanza kufundishwa kama somo la hiari katika ngazi ya chuo kikuu nchini Tanzania. Kutokana na hili, Mahakama ya Rufaa, Mahakama kuu na Mahakama zote nchini hazikuwa na Majaji na Maofisa wa Mahakama wenye ujuzi katika sheria ya mazingira. Hali hii iliathiri upinzani wa kisheria katika mashauri ya kimazingira. Ni muhimu kufahamu kwamba, nje ya mashauri ya kimazingira kuhusu alama za mipaka ya ardhi yaliyobishaniwa mahakamani mwaka

1991[34] na 2000[35] hakuna shauri la kisheria la maana lililojengwa kwenye sheria ya mazingira nchini Tanzania.

Katika yote vifungu vya kisheria vilivyoainishwa kwa uwazi na kwa umakini vilivyopo kwenye EMA vinavyohusu uhifadhi na menejimenti ya mazingira pamoja na haki ya mazingira masafi na yenye afya vinahitaji viwe na mizizi yao katika itakayokuwa katiba mpya ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

## 7.0 Tuliyojifunza Kutoka katika Katiba za Nchi Zilizochaguliwa

Katiba kutoka Afrika na nchi zilizoendelea ambazo zina vifungu kuhusu haki za mazingira, uhifadhi na menejmenti ya mazingira zipo nyingi. Hili pitio linachambua sampuli iliyochaguliwa miongoni mwao ili tujifunze kutokana na uzoefu wao kwa lengo la kuainisha yale yatakayofaa kuingizwa kwenye mchakato wa utayarishaji wa Katiba mpya Tanzania. Katika kujifunza kutoka katiba za nchi nyingine, tutazingatia tofauti ya hali zilizopo za kijamii, kiuchumi, kitamaduni, na kisiasa katika nchi hizo na Tanzania.

Kwa kuanzia, Katiba ya Jamhuri ya Kenya imeainisha kwa umakini na kwa undani masuala yanayohusu mazingira. Wananchi wa Kenya wameingiza katika Katiba yao sura pekee (sura ya tano) ikijikita katika mambo yanayohusu Ardhi na Mazingira. Sura hii imegawanywa katika sehemu mbili. Sehemu ya kwanza inajikita kwenye mambo ya ardhi na sehemu ya pili hii inajikita kwenye mambo ya mazingira na maliasili. Katika mambo yanayohusu mazingira yaliyopo sehemu ya pili ya Sura ya Tano na Ibara nyingine za Katiba ya Jamhuri ya Kenya, masuala ya kimazingira yamewekwa wazi na kuelezwa kwa kina.

Chini ya Ibara ya 42, haki ya mazingira masafi na yenye afya inasisitizwa. Inaelezwa kuwa," Kila mtu ana haki ya kuwa na mazingira masafi na yenye afya, inayojumuisha haki ya - (a) Kuwa na mazingira yanayohifadhiwa kwa manufaa ya kizazi cha sasa na kijacho kwa mujibu wa sheria na hatua nyinginezo; (b) wajibu wa yanayohusu mazingira kutimizwa"

[34] Festo Balegele and 794 Others v. Dar es Salaam City Council, High Court of Tanzania at Dar es Salaam, Miscellaneous Civil Case, No. 90 of 1991.

[35] Felix Joseph Mavika v. Dares Salaam City Commission, High Court of Tanzania at Dares Salaam, Miscellaneous Civil Case, No.316 of 2000

Katiba ya Jamhuri ya Kenya inaenda hatua ya mbele zaidi kwa kutoa wajibu unaotakiwa kuzingatiwa, inaweka majukumu kuhusu mazingira na haki za kimazingira zinazotambuliwa na kuhifadhiwa na Katiba, endapo inaelekea au yapo katika hati hati ya kukataliwa, kukiukwa, kukoseshwa au kutishiwa. Chini ya ibara ya 69 (1) wajibu kuhusu menejimenti ya mazingira na uhifadhi wake umetolewa. Hili jukumu la jumla limetolewa kwa Dola. Katiba inasema kuwa serikali / dola - (a) itahakikisha uchimbaji endelevu, matumizi, menejimenti na uhifadhi wa mazingira na maliasili, na kuhakikisha kwamba kunakuwepo na usawa katika mgawo wa faida / manufaa zitokanazo; (b) itafanya kazi ili kufikia na kudumisha ujazo wa miti wa angalau asilimia kumi ya ardhi ya Kenya; (c) itatunza na kuendeleza mali zitokanazo na akili, ujuzi wa kiasili wa viumbe hai vya aina mbalimbali na rasilimali za kijenetiki (viini nasaba / kizazi) za jamii; (d) itahimiza ushiriki wa umma katika menejimenti, ulinzi na uhifadhi wa mazingira; (e) italinda rasilimali za kijenetiki na viumbe hai vya aina mbalimbali; (f) itatengeneza mifumo ya kutathmini athari, ukaguzi na ufuatiliaji wa mazingira; (g) itaondoa mlolongo wa mambo na shughuli ambazo zinaweza kuhatarisha mazingira na (h) itatumia mazingira na maliasili kwa manufaa ya watu wa Kenya.

Jukumu la raia kulinda, kuhifadhi, kutunza na kusimamia mazingira imetolewa chini ya kipengele cha 2 cha Ibara ya 69. Hii inatamka kuwa," Kila mtu ana wajibu wa kushirikiana na vyombo vya dola na watu wengine kulinda na kuhifadhi mazingira na kuhakikisha maendeleo endelevu ya kiekolojia na matumizi endelevu ya maliasili".

Katiba ya Jamhuri ya Ghana inachukulia uhifadhi na menejimenti ya mazingira kama hitaji la awali kwa maendeleo ya taifa kiuchumi na kwa uimarishaji wa hali ya maisha ya watu wa Ghana. Inatoa jukumu kwa serikali na kwa wananchi kuchukua hatua stahiki kuhifadhi na kulinda mazingira kwa ajili ya vizazi vya sasa na vya baadaye. Inatamka kuwa," Dola itachukua hatua stahiki zinazohitajika kuhifadhi na kulinda mazingira ya taifa kwa ajili ya ustawi; na itatafuta ushirikiano na nchi zingine na vyombo vingine kwa ajili ya kulinda uwanda mpana wa kimataifa wa mazingira kwa ajili ya binadamu[36].

[36] Ibara ya 36 (9) ya Katiba ya Jamhuri ya Ghana

Katiba ya Jamhuri ya Afrika ya Kusini ina kifungu kinachotoa haki za mazingira na wajibu wa kuhifadhi, kutunza na kusimamia mazingira. Inatamka kuwa," kila mmoja ana haki [37] (a) ya kuwa na mazingira ambayo hayana madhara kwa afya zao na uwepo wao mzuri; na (b) ya kuwa na mazingira yanayohifadhiwa, kwa manufaa ya vizazi vya sasa na vya baadaye kwa kupitia sheria zinazofaa na hatua nyingine ambazo:- (i) zinazuia uchafuzi na uharibifu wa ekolojia; (ii) zinahimiza uhifadhi; na (iii) zinaleta maendeleo endelevu ya kiekolojia na matumizi ya maliasili wakati huo huo zikihimiza maendeleo thabiti ya kiuchumi na ya kijamii". Katiba hii inaenda hatua zaidi kwa kutamka kwamba miongoni mwa malengo ya serikali ya mtaa ni" kuhimiza mazingira salama na yenye afya[38]."

Katiba ya Jamhuri ya Uganda[39] imetenga sura ya kumi na tano kwa ajili ya mambo yanayohusu ardhi na mazingira. Inaeleza kwa makusudi kabisa kwamba ardhi ni mali ya watu wa Uganda na itamilikishwa kwao kwa mujibu wa mfumo wa umilikishaji wa ardhi uliopo kwenye Katiba. Pia inaelekeza kuhusu uundaji na shughuli za taasisi zenye mamlaka ya kupanga taratibu za menejimenti ya ardhi na utawala wake. Kuhusu uhifadhi na menejimenti ya mazingira Katiba inathibitisha kuwa Bunge kisheria itaelekeza mbinu zenye makusudi ya:- (a) kulinda na kuhifadhi mazingira dhidi ya matumizi mabaya, uchafuzi na uharibifu; (b) kutunza na kusimamia mazingira kwa maendeleo endelevu; (c) kuhimiza ufahamu wa mazingira Katiba imeacha mambo muhimu kuhusu haki za mazingira, hifadhi na menejimenti ya mazingira nchini Uganda kushughulikiwa na sheria ya mazingira.

Katiba ya Iraq [40] inasisitiza juu ya haki ya kuishi katika mazingira masafi na yenye afya na ulinzi na uhifadhi wa viumbe hai vya aina mbalimbali. Chini ya Ibara ya 33 kuna tamko kwamba "Kwanza: Kila mtu binafsi ana haki ya kuishi katika hali ya mazingira salama. Pili: Serikali itashughulikia utunzaji na uhifadhi wa mazingira na viumbe hai vya aina mbalimbali. Katiba inatoa jukumu kwa serikali ya shirikisho na ya majimbo kutayarisha sera ya mazingira kuhakikisha ulinzi wa mazingira dhidi ya uchafuzi na kuhifadhi usafi wake kwa ushirikiano na majimbo na tawala nyingine zisizo za kijimbo[41].

---

[37] Ibara ya 24 ya Katiba ya Jamhuri ya Afrika ya Kusini
[38] Ibara ya 152, ya Katiba ya Jamhuri ya Afrika ya Kusini
[39] Katiba ya Uganda, Iliyorekebishwa na sheria ya katiba (marekebisho) 11/2005 na (marekebisho) ya sheria (Na 2) ya 21/2005
[40] http;//www.uniraq.org/documents/Iraqi_constitution.pdf
[41] Ibara ya 114 ya Katiba ya Iraq

Hatuhitaji hata kusema kwamba, katiba zote tulizozipitia hapo juu zina vifungu vilivyo wazi vinavyotoa mamlaka kwa serikali na raia kulinda, kuhifadhi, kutunza na kusimamia mazingira. Pia zinatoa misingi ya sheria ambayo kutokana nayo haki za kimazingira zinaweza kudaiwa na kutetewa mara tu zinapoanza kukiukwa.

Zaidi ya hayo, uchambuzi makini wa vifungu vya Katiba tulizopitia, unaonyesha kwamba mazingira na maliasili zitatumika nchini Kenya, Ghana, Afrika Kusini, Uganda na Iraq kwa maendeleo ya kijamii na kiuchumi kwa manufaa ya wananchi. Kwa kuangalia yaliyomo katika vifungu vya Katiba hizo za kigeni hapo juu, kwa hiyo ni muhimu sana kwa Tanzania kuingiza katika itakayokuwa Katiba mpya vifungu vitakavyowezesha azma hii. Watanzania wamekuwa wakitetea matumizi bora na endelevu ya mazingira na maliasili kwa lengo la kuimarisha hali zao za maisha kijamii na kiuchumi. Hii Kampeni na kazi ya utetezi katika matumizi ya maliasili kwa manufaa ya raia wa Tanzania, bado haijaleta ushindi.

## 8.0 Majumuisho na Mapendekezo

### (a) Majumuisho

Mamlaka na wajibu wa kulinda, kuhifadhi, kutunza na kusimamia mazingira kwa ajili ya kizazi cha sasa na cha baadaye ni wa umuhimu mkubwa kwa ustawi wa Watanzania, maendeleo ya kijamii na ya kiuchumi. Umuhimu huu unataka uingizaji wa wazi wa vifungu hivyo katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ili kutoa msingi imara wa kuhimiza utekelezaji wake. Kwa hali hii, sasa wakati umefika kwa Watanzania kufungamanisha haki za mazingira, misingi ya menejimenti ya mazingira na wajibu wa kulinda, kuhifadhi, kutunza na kusimamia mazingira katika katiba.

### (b) Mapendekezo

Kwa kuzingatia mapitio yaliyofanywa katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na rejea iliyofanywa kwenye Katiba za nchi kadhaa zilizochaguliwa mapendekezo yafuatayo yanatolewa:-

(i) Kuna hitaji la kuingiza katika Katiba ya Jamhuri ya Mungano wa Tanzania vifungu vilivyoainishwa kwa umakini, kwa uwazi na vinavyotoa mamlaka ya ulinzi, uhifadhi, utunzaji na usimamizi wa mazingira Tanzania kwa serikali na wananchi

(ii) Inapendekezwa kwamba masuala ya haki ya kuishi katika mazingira safi, salama na yenye afya, misingi ya menejimenti endelevu ya mazingira, majukumu na wajibu wa kulinda, kuhifadhi, kutunza na kusimamia mazingira sharti yaingizwe katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; na

(iii) Inapendekezwa kuwa kifungu kinachosisitiza matumizi ya mazingira na maliasili kwa manufaa ya Watanzania kinaingizwa katika katiba mpya.

## 9.0 BIBLIOGRAFIA (BIBLIOGRAPHY)

### a) Vitabu, Jarida na Taarifa (Books, Articles and Reports)

Bruch, C., et al, (2001), "Breathing Life into Fundamental Principles: Implementing Constitutional Environmental Protections in Africa", in Ribot, J. C. and Veit, P. G., Environmental Governance in Africa, Working Paper Series, World Resources Institute, Washington D.C., USA.

Tumushabe, G.W., (1999), "Environmental Governance, Political Change and Constitutional Development" in Uganda in Okoth-Ogendo, H. W. O. and Tumushabe, G.W., (Eds), Governing the Environment: Political Change and Natural Resources Management in Eastern and Southern Africa, African Centre for Technology Studies (ACTS), Nairobi, Kenya.

Laltaika, E., (2011), "Call to include Environmental Rights in the Constitution", the Citizen Newspaper, 22 June 2011.

### b) Katiba (Constitutions)

Katiba ya Jamhuri ya Afrika ya Kusini

Katiba ya Jamhuri ya Ghana.

Katiba ya Jamhuri ya Kenya.

Katiba ya Jamhuri ya Iraq.

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Katiba ya mwaka 1977 (kama ilivyorekebishwa muda baada ya muda)

Katiba ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Watu wa Algeria, 1989 (iliyorekebishwa kwa mapitio ya Katiba ya 1996)

Katiba ya Uganda, iliyorekebishwa kwa sheria ya marekebisho ya Katiba 11/2005 na sheria ya marekebisho ya katiba Na.2 ya 21/2005.

**c) Vifungu vya Sheria**

Sheria ya Menejimenti ya Mazingira, Na. 20 of 2004.

Sheria ya Misitu ya 2002

Sheria ya Ardhi, sura ya 113.

Sheria ya Wanyama Pori, sura ya 283

Sheria ya Madini, sura ya 123.

Sheria ya kijiji kuhusu Ardhi . 114.

**d) Tovuti (Websites)**

http://www.state.gov/r/pa/ei/bgn/2843.htm

http://www.worldsummit2002.org/index.htm?http://www.worldsummit2002.

org/guide/stockholm.htm

http://www.un.org/geninfo/bp/enviro.html

http://www.uniraq.org/documents/iraqi_constitution.pdf

http://pdf.wri.org/eaa_bruch.pdf

http://www2.ohchr.org/english/issues/environment/environ/bp4.htm

**e) Mashauri (Cases)**

Festo Balegele and 794 Others vs. Dar es Salaam City Council, High Court of Tanzania at Dar es Salaam, Miscellaneous Civil Case, No. 90 of 1991.

Felix Joseph Mavika v. Dar es Salaam City Commission, High Court of Tanzania at Dar es Salaam, Miscellaneous Civil Case No. 316 of 2000.

Maneka Gandhi v. Union of India, AIR 1978 SC 597, 623-624.

Charan Lal Sahu v. Union of India, AIR 1990 SC 1480.

Subhash Kumar v. State of Bihar, AIR 1991 SC 420/ 1991 (1) SCC 598.

LAWYERS ENVIRONMENTAL ACTION TEAM (LEAT)

SHERIA NA ULINZIWA MAZINGIRA

policy forum